**TAARIFA KWA UMMA ILIYOTOLEWA NA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA, DKT SELEMANI JAFO, KUHUSU UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA KANUNI NA MWONGOZO WA BIASHARA YA KABONI, 16 DISEMBA, 2022, DODOMA**

**Ndugu wanahabari,**

Awali ya yote nipende kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutukutanisha mahali hapa leo kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma kuhusu hatua ambazo Serikali imezichukua katika kuboresha uratibu na kuleta ufanisi katika jitihada mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo kuandaa Kanuni na Mwongozo wa Biashara ya Kaboni hapa nchini.

Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na masuala Mengine imepewa jukumu la kuratibu jitihada za wadau katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo uratibu wa Biashara ya Kaboni ambayo inalenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto ambayo ndio kiini cha athari hasi za mabadiliko ya tabianchi.

**Ndugu wanahabari,**

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoathiriwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa isiyotabirika. Hali hii inajidhihirisha kupitia matukio ya mvua zisizotabirika, ongezeko la joto, ukame na mafuriko. Athari hizi za mabadiliko ya tabianchi zimeathiri sekta za kijamii na kiuchumi na maendeleo kama vile kilimo, utalii, nishati, maji, afya, mifugo na mifumo ikolojia ya bahari na ardhi, hivyo kuathiri ongezeko la pato la taifa. Aidha, ukame wa muda

mrefu na mafuriko yamechangia gharama kubwa za kiuchumi, kuathiri maendeleo na maisha ya jamii za vijijini na mijini.

**Ndugu wanahabari,**

Jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabainchi zimeibua changamoto na fursa muhimu ambazo zinaweza kusaidia kuchochea uhifadhi na maendeleo endelevu. Katika kuhakikisha changamoto zinaondelewa na fursa zilizopo zinakuwa na manufaa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na; mapitio ya sera, uandaaji wa kanuni, mikakati na miongozo ya kukabiliana na changamoto zinazotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Ndugu wanahabari,**

Biashara ya Kaboni ni mojawapo ya nyenzo muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi duniani**.** Biashara hii hufanyika miongoni mwa nchi wanachama wa Makataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi Mwanachama wa mikataba hii. Hivyo, pamoja na sera na mikakati iliyopo na kwa kuzingatia umuhimu wa Baishara hii, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa Kanuni na Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini. Malengo makuu ya Kanuni na Mwongozo huu ni kuweka utaratibu na masharti ambayo wadau na wajasiriamali wa biashara ya kaboni watapaswa kuzingatia wakati wa utekelezaji wa miradi mipya na miradi inayoendelea ya biashara ya kaboni katika sehemu mbalimbali ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kanuni na mwongozo zinalenga kuweka mazingira rafiki ya usimamizi wa mazingira na biashara nchini. Kanuni na na Mwongozo tayari zimekwisha sainiwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 636 na 637 la tarehe 28 Oktoba, 2002. Hivyo, kuwa tayari kwa matumizi.

**Ndugu wanahabari,**

Kanuni na Mwongozo wa Usimamizi wa Biashara ya Kaboni zimejikita katika kuimarisha mchango wa nchi katika jitihada za kupunguza uzalishaji wa gesijoto na hivyo kupunguza athari za mazingira kwa kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kwa kuzingatia misingi ya maendeleo endelevu, utunzaji endelevu wa mazingira, ushiriki wa jamii, uwazi, ufanisi, ujumuishaji wa faida za kijamii, kiuchumi na mazingira, na uzingatiaji wa viwango vya kimataifa. Aidha kanuni hizo zinalenga kuhakikisha kuwa jamii, wadau mbalimbali wanaohusika na biashara hiyo ikiwa pamoja na Serikali kunufaika kikamilifu kutokana na faida zilizopo katika biashara ya kaboni nchini.

**Ndugu wanahabari,**

Uzingatiaji na utekelezaji wa Kanuni na Mwongozo wa Biashara ya Kaboni utasaidia kuboresha usimamizi mzuri wa miradi ya biashara ya kaboni inayotekelezwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sekta zote. Hivyo, utekelezaji wa biashara ya kaboni utachangia kupunguza gesijoto zinazosababisha ongezeko la joto duniani na hatimae kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kuchangia katika utunzaji endelevu ya mazingira na kuleta maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Aidha, uzingatiaji na utekelezaji wa Kanuni na Mwongozo wa Usimamizi wa Biashara ya Kaboni ni jukumu la wadau wote, ikiwemo Wawekezaji wa Kimataifa na wanaotoka ndani ya nchi, Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa .

**Ndugu wanahabari,**

Wakati wa kuandaa Kanuni na Mwongozo, tunatambua kuwa kuna baadhi ya miradi ya baishara ya Kaboni ambayo tayari ilikuwa inaendelea katika baadhi ya

maeneo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, rai yangu ni kusihi wawekezaji, wananchi na watu wote wanaohusika na utekelezaji wa miradi hiyo waanze mara moja kuhuisha miradi yao na kujisajili upya kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Kituo cha Ufuatiliaji wa Kaboni kilichopo Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro ili iendane na matakwa ya kanuni na mwongozo uliopo. Hivyo, naelekeza Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Kituo cha Ufuatiliaji wa Kaboni na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika Kanda zote kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wa maendeleo kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa Kanuni na Mwongozo wa Usimamizi wa Biashara za Kaboni.

**Ndugu wanahabari,**

**Kwa kumalizia,** nipende tena kuwashukuru kwa kuitikia wito na ni matumaini yangu kuwa nanyi wanahabari mtaendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa uzingatiaji na utekelezaji wa Kanuni na Mwongozo wa Usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**